

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**HALMASHAURI YA WILAYA YA NJOMBE**  
*(Mawasiliano yote yafanywe kupitia kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya*

Simu Na.: 2782111 Mkurugenzi  
Fax Na. 0262782857  
Website : [www.njombedc.go.tz](http://www.njombedc.go.tz)  
E-mail: [ded@njombedc.go.tz](mailto:ded@njombedc.go.tz)



S.L.P 547,  
**NJOMBE.**  
11 Machi, 2021

**TAARIFA KWA UMMA**

**TANZIA**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe anasikitika kutangaza kifo cha Bi. Elitha .J. Mligo aliyekuwa mkuu wa idara ya Kilimo, umwagiliaji na ushirika katika Halmashauri ya wilaya ya Njombe. Kifo hicho kimetokea leo tarehe 11 Machi, 2021 katika Hospitali ya Taifa Muhimbili alipokuwa akipata mtibabu.

Marehemu alikuwa mtumishi wa taasisi hii tangu mwaka 1986 alipoajiriwa kama Afisa Kilimo na baadae mwaka 2007 alipandishwa cheo na kuwa mkuu wa idara hiyo.

Kwa niaba ya Uongozi na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe natoa pole kwa familia ya marehemu, Waheshimiwa Madiwani, uongozi, Watumishi na wananchi wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe kwa kuondokewa na mtumishi wao.

Taarifa zaidi kuhusu taratibu za mazishi zitaendelea kutolewa na uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Njombe. Bwana ametoa na Bwana ametwaa, jina la Bwana lihimidiwe. Amina.

Tangazo hili limetolewa na

Mkurugenzi Mtendaji,  
**Halmashauri ya Wilaya ya Njombe**